# KUTOKA BUSTANINI HADI KWENYE KABURI TUPU

Kutoka kwenye Bustani ya Gethsemane hadi kwenye kaburi tupu, Pasaka inawakilisha muda wa ndani zaidi katika historia ya mwanadamu – utimilifu wa mpango wa ukombozi wa Mungu kupitia kwa kifo na kufufuka kwa Yesu Kristo. Tunapotafakari kuhusu huu msimu mtakatifu, tunashuhudia upendo wa Mungu ukikishinda kifo chenyewe, ukitoa kwa mwanadamu zawadi kubwa zaidi ya kufikirika: wokovu wa milele kupitia kwa Bwana wetu aliyefufuka.

'Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.' (Yohana 3:16). Kifungu hiki maarufu kinachukua maana inayofanywa mpya mara tena tunaposafiri katika matukio ya Juma Takatifu, tukielewa undani wa sadaka ambayo upendo wa Mungu ulihitaji.

Njia ya Pasaka inaanzia katika kivuli cha usaliti. Katika bustani ya Gethsemane, Yesu alionyesha ukamilifu wa kujitoa kwa kusudi la Baba, hata wakati nafsi yake ikiwa 'imezidiwa na huzuni kiasi cha kufa' (Marko 14:34). Licha ya Kristo kutambua mateso yaliyokuwa yanamsubiria, maombi yake yalidhihirisha utii usioyumbishwa. 'Walakini, si kama nitakavyo mimi, bali utakavyo wewe' (Marko 14:36). Kipindi hiki cha kujitoa kwa hali ya juu kinatufundisha sisi kwamba imani ya kweli maana yake ni kuuamini mpango wa Mungu hata katika saa zetu za giza nene.

Tukio lililofuata – kesi ya dhihaka, kupigwa mijeredi kikatili na safari ya kwenda Golgotha – inadhihirisha undani wa dhambi ya mwanadamu na urefu wa upendo wa Mungu. Kama vile Isaya alivyotabiri karne nyingi mapema, 'Bali alijeruhiwa kwa makosa yetu, alichubuliwa kwa maovu yetu; Adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake, na kwa kupigwa kwake sisi tumepona' (Isaya 53:5). Kila mjeredi, kila mwiba, kila msumari unatoa ushuhuda wa gharama ya ukombozi wetu.

Pale Kalwari, tunashuhudia vyote, hofu ya dhambi na maajabu ya neema. Msalaba unasimama kama alama ya mwisho ya upendo unaojitoa sadaka, mahali ambapo Mwana wa Mungu asiye na dhambi alibeba uzito wote wa uvunjaji sheria wa mwanadamu. 'Yeye asiyejua dhambi alimfanya kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate kuwa haki ya Mungu katika Yeye' (2 Wakorintho 5:21). Kama Yesu alivyotangaza 'Imekwisha' (Yohana 19:30), alitimiza kila unabii, akatosheleza kila haki ya Mungu, na akajenga daraja juu ya shimo lililokuwa kati ya Mungu na mwanadamu.

Lakini Msalaba sio mwisho wa hadithi. Kama kifo cha Kristo kingekuwa ukurasa wa mwisho, imani yetu ingekuwa bure. Kama Paulo alivyoandika: 'Tena kama Kristo hakufufuka, basi, kuhubiri kwetu ni bure na imani yetu ni bure' (1 Wakorintho 15:14). Ufufuo unabadilisha kila kitu. Wakati Mariamu Magdalena na wanawake wengine walipokaribia kwenye kaburi mapema Jumapili asubuhi, waligundua muujiza mkubwa katika historia – jiwe lilikuwa limevingirishwa na kifo kimeshindwa.

Tangazo la malaika linaimba katika vizazi vyote: 'Hayupo hapa; kwani amefufuka,kama alivyosema.' (Mathayo 28:6). Maneno haya yalibadilisha mwelekeo wa historia ya mwanadamu na yanaendelea leo kubadilisha maisha. Ufufuo unathibitisha kila dai alilolitoa Yesu kuhusu utambulisho na utume wake. Unathibitisha kwamba yeye kweli ni Mwana wa Mungu, mwenye uwezo juu ya kifo chenyewe. Kama Warumi 1:4 inavyosema, 'na kudhihirishwa kwa uweza kuwa Mwana wa Mungu, kwa jinsi ya roho ya utakatifu, kwa ufufuo wa wafu, Yesu Kristo Bwana wetu'.

Matokeo ya ufufuo ni makubwa na ni ya binafsi. Kwa sababu Kristo anaishi, sisi pia tutaishi. Ushindi wake unakuwa ushindi wetu, maisha yake maisha yetu. 'Lakini sasa Kristo amefufuka katika wafu, limbuko lao waliolala' (1 Wakorintho 15:20). Ufufuo unathibitisha kwamba kifo hakina tena uchungu wake na kaburi limeshindwa. Tunamtumikia Mwokozi anayeishi anayeahidi 'Kwa sababu mimi ni hai, ninyi nanyi mtakuwa hai' (Yohana 14:19).

Asubuhi ya Pasaka inakaribisha uumbaji mpya. Nguvu iliyomwinua Kristo kutoka kwa wafu ndiyo nguvu ile ile inayobadilisha leo maisha ya waamini. Kama Paulo anavyoeleza: 'Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya, ya kale yamepita, tazama! yamekuwa mapya' (2 Wakorintho 5:17). Ufufuo sio tu tukio la kihistoria la kusherehekea – bali ni ukweli uliopo unaotoa tumaini, kusudi na maisha mapya kwa wote wanaoamini.

Ushindi wa Pasaka hii unakwenda zaidi ya wokovu wa mtu binafsi hadi kwenye umuhimu wa ulimwengu. Ufufuo wa Kristo unaanzisha kurejeshwa kwa uumbaji wote, Mungu anapoanza kuvifanya vyote kuwa vipya. Kaburi tupu linatangaza kwamba dhambi, kifo na Shetani ni maadui walioshindwa. Ingawa bado tunapambana dhidi ya uovu katika kizazi hiki cha sasa, vita kwa uamuzi tayari ushindi umepatikana. Kama Paulo anavyotangaza kwa ushindi: 'Lakini Mungu na ashukuriwe atupaye kushinda kwa Bwana wetu Yesu Kristo' (1 Wakorintho 15:57).

Ufufuo vile vile unawawezesha waamini kwa ajili ya utumishi wa Kikristo. Roho yule yule aliyemfufua Kristo kutoka kwa wafu anaishi ndani ya waamini, akituwezesha kuishi kwa ushindi na kutumika kwa ufanisi. Kama Paulo alivyoomba, tunaweza kufahamu 'ubora wa ukuu wa uweza wake ndani yetu tuaminio jinsi ulivyo, kwa kadiri ya utendaji wa nguvu za uweza wake, aliotenda katika Kristo alipomfufua katika wafu, akamweka mkono wake wa kuume katika ulimwengu wa roho' (Waefeso 1:19-20).

Kristo aishiye anatuagiza sisi tuushirikishe habari hii njema ulimwengu unaohitaji mno tumaini. Wanawake pale kaburini walipokea mamlaka ya kwanza ya uinjilisti: 'Nanyi nendeni upesi, mkawaambie wanafunzi wake, amefufuka katika wafu' (Mathayo 28:7). Agizo hilo linasambazwa kwa waamini wote leo. Sisi ni mashahidi wa ufufuo huu, tulioitwa kuutangaza ujumbe wa Pasaka kwenye kona zote za dunia.

Majira haya ya Pasaka, hebu tumfurahie Bwana wetu aliyefufuka aliyeshinda kifo na akatupatia wokovu wetu wa milele. Hebu tukumbatie uweza wa ufufuo wake katika

maisha yetu ya kila siku, huku tukiruhusu ushindi wake ubadilishe kushindwa kwetu kuwe kushinda. Tunaposherehekea kaburi tupu, hebu turudie kwa sauti maneno ya salamu ya zamani ya Wakristo: Amefufuka! Amefufuka kwa kweli!'.

Uzuri wa Pasaka haumo tu katika matukio ya historia tunayoadhimisha, bali katika uweza unaoendelea wa kubadilisha maisha leo. Kwa sababu anaishi, tunaweza kukabiliana na kesho kwa ujasiri, huku tukifahamu kwamba hakipo kinachoweza kututenganisha na upendo wake. Kama Paulo anavyotangaza: 'Lakini katika mambo hayo yote tunashinda, na zaidi ya kushinda, kwa yeye aliyetupenda. (Warumi 8:37).

Naomba Pasaka hii mioyo yetu ijazwe furaha mpya katika Mwokozi wetu aliyefufuka, shukurani za kina kwa ajili ya kujitoa kwake na tujitoe upya kwa ajili ya utumishi wake. Kaburi litupu, kifo kimeshindwa na Kristo anatawala kwa ushindi. Huu ndiyo utukufu wa Pasaka – sio tu ni tukio lililopita, bali ukweli wa wakati huu unaotoa tumaini, kusudi na maisha ya milele kwa wote wanaomwamini Bwana aliyefufuka.

'Basi, Mungu wa amani aliyemleta tena kutoka kwa wafu Mchungaji Mkuu wa kondoo, kwa damu ya agano la milele, yeye Bwana wetu Yesu, awafanye ninyi wakamilifu katika kila tendo jema, mpate kuyafanya mapenzi yake, naye akifanya ndani yetu lipendezalo mbele zake, kwa Yesu Kristo, utukufu una yeye milele na milele. Amina' (Waebrania 13:20-21).

**Lyndon Buckingham**
**General**